

**LEAD
LEAD**



FOUNDATION

zubauza

PROGRAMU YA KUKIJANISHA MKOA WA DODOMA

REGREENING DODOMA REGION PROGRAMME

2017 - 2022

MADHUMUNI YA PROGRAMU

- Kuikomboa ardhi iliyochakaa ya mashamba na malisho izalishe chakula na malisho kwa wingi ili kupambana na baa la njaa;**
- Kukuza kilimo-misitu na njia nyingine za kilimo na ufugaji bora;**
- Kumletea mkulima mlangoni kwake nishati za mkaa na kuni na mazao mengine ya miti (kama ufugaji wa nyuki) ambayo yataongeza pato la kaya na kuondoa uvamizi wa misitu iliyohifadhiwa;**
- Kuongeza uwezo wa jamii na serikali zao kutunza mazingira na mali asili ili kuboresha maisha na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.**
- Kuwezesha jamii kujipatia maji kwa njia rahisi za uvunaji wa maji.**

MADHUMUNI YA PROGRAMU



hamisi_kigwangalla
Babati





2,059 likes

hamisi_kigwangalla Ili jitihada zetu za kujenga taifa endelevu zifanikiwe, ni lazima tuwekeze zaidi kwenye kuwafundisha na kuwawezesha wananchi wenzetu kuzalisha nishati yao wenyewe, fito na mbao zao kwa ajili ya ujenzi, malisho yao kwa ajili ya mifugo yao, na siyo kutegemea maeneo ya hifadhi! #HK #MzeeWaField #TanzaniaUnforgettable #NjeYaBox

MALENGO

- 1. Kufikia 50% ya kaya za Mkoa wa Dodoma katika wilaya zote 7 ifikapo mwaka 2022 = Kaya 180,000**



MALENGO

2. Kukomboa hekta 180,000 kwa miti ya Kisiki Hai



MALENGO

3. **Kustawisha miti milioni 14 kwa kutumia njia ya Kisiki Hai**

MALENGO

Miaka 4 Awamu 5

2017	2018				2019				2020				2021				2022		
Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	Q3	Q4	Q1	Q2	
	Stage 1: K (yr 1)																		
		Stage 2: KMCB (yr 1)																	
							Stage 3: KMCB (yr 2)												
							Stage 3: DKC (yr 1)												
											Stage 4: KMCB (yr 3)								
											Stage 4: DKC (yr 2)								
															Stage 5: DKC (yr 3)				

MALENGO MPWAPWA

- 1. Tarafa 2 za Rudi na Mpwapwa;**
- 2. Kata zote na Vijiji vyote vitafikiwa katika tarafa hizi (Kata 19, Vijiji 54);**
- 3. Kaya 37,000 zitafikiwa;**
- 4. Kustawisha miti 2,960,000 kwa njia ya Kisiki Hai;**
- 5. Kuhamasisha kilimo cha zao la KOROSHO katika vijiji vyote tutakavyofikia.**



MKAKATI WA UTEKELEZAJI

- 1. Kuwasilisha Programu hii kwa Viongozi na wadau wote wa ngazi za Mkoa na Wilaya (Advocacy) ili kupata ridhaa yao na mshikamano wao katika kuhakikisha mafanikio yanapatikana kwa wakati.**



MKAKATI WA UTEKELEZAJI

- 2. Wanakijiji wanne (4) kutoka kila kijiji watapewa mafunzo ya kina (ToT Training) kuhusu njia ya Kisiki Hai ili wawe walimu wa wanakijiji wenzao (Machampioni wa Kisiki Hai wa Vijiji).**



MKAKATI WA UTEKELEZAJI

- 3. Kuhamasisha wananchi katika kila kijiji kupitia mikutano, makongamano na njia nyingine ikiwemo kuonesha filamu ya Kisiki Hai katika kila kijiji (Video Caravan).**



MKAKATI WA UTEKELEZAJI

- 4. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) katika kila kijiji ili kujua maendeleo ya programu ikiwemo idadi ya miti iliyostawishwa pamoja na kutatua changamoto zitakazojitokeza.**



MKAKATI WA UTEKELEZAJI

5. **Kufanya Harakati (Movement) mijini na vijijini ili kuhamasisha wananchi na wadau mbalimbali kuunga mkono juhudi zetu za kutunza mazingira na kukijanisha mkoa wetu na nchi yetu kwa ujumla.**



MKAKATI WA UTEKELEZAJI

- 5. Kufanya Ubunifu (Innovation) pamoja na kuibua miradi mingine itakayosaidia kuboresha Programu ya Kisiki Hai kama mradi wa Ufugaji wa Nyuki pamoja na mradi wa Kukinga Maji ya Mvua Pembamoto.**



WASHIRIKA WENZA

Programu hii inatarajiwa kutekelezwa kwa kushirikiana na Mashirika na Taasisi mbalimbali likiwemo Shirika la Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la “Justdiggit” kutoka Uholanzi pamoja na Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya.



KISIKI HAI NI NINI

Kisiki Hai ni njia ya kustawisha miti kwa kutunza uoto wa asili; kwa Kiingereza inaitwa Farmer Managed Natural Regeneration (FMNR). Njia hii inahusu kuchagua na kupogolea machipukizi ya visiki vya miti iliyokatwa zamani ambavyo havijakauka na kufa kabisa, au maotea ya miti yanayotokana na mbegu zilizodondoshwa na upepo, kinyesi cha wanyama au ndege.


Kuna mamilioni ya visiki hai na maotea ya miti kwenye mashamba, maeneo ya malisho na sehemu nyingi za misitu iliyoharibiwa kwa ukataji miti.

KISIKI HAI NI NINI

Kisiki Hai ni njia ya kuruhusu msitu ulio chini ya ardhi utokeze na kuleta mabadiliko makubwa katika ardhi na mazingira kwa jumla. Njia hii ni rahisi zaidi ikilinganishwa na ile ya kupanda miti hasa katika mikoa yenye uhaba wa mvua, kama Dodoma.

MACHIPUKIZI YA KISIKI HAI

MIZIZI YA KISIKI HAI



FAIDA KUBWA ZA NJIA HII

- Gharama nafuu kwa vile haihitaji utafutaji wa miche au umwagiliaji maji.**
- Uwezo wa kukomboa maeneo makubwa yaliyoathirika na uharibifu wa mazingira kwa muda mfupi.**
- Ni rahisi kutekelezwa.**
- Ni endelevu**

HITIMISHO

Ili Shirika liweze kufikia malengo yake, tunahitaji zaidi ushirikiano wa Serikali katika ngazi zote, kuanzia ngazi ya Mkoa hadi kijiji. Lengo ni kuona kwamba utekelezaji wa mradi huu unafanikiwa kwa kiwango cha juu kabisa kwa faida ya Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Kisiki Hai ni Mkombozi wa Mazingira!

Kijanisha Dodoma Iwe Poa!

ASANTENI

KWA MAWASILIANO

Kitalu No. 125 Kilimani

S.L.P 1823 Dodoma

Simu: 026 2322786

Barua pepe: info@leadfoundation.or.tz

Tovuti: www.leadfoundation.org

 LEAD Foundation

 @leadtz